

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO
AnwaniyaSimu:REGCOM, KILIMANJARO
Simu Na: +255 (027) 2754236/7
NUKUSHI: +255(027) 2752184
Barua Pepe: ras@kilimanjaro.go.tz
: ras.kilimanjaro@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,
S.L.P.3070,
MOSHI.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tarehe 24/04/2020, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro Dkt.Khatibu Kazungu alifanya ziara katika vijiji vya kituri na kileo vilivyopo katika Wilaya ya Mwanga. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kujionea hali halisi pamoja na athari zilizosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika Mkoa wa Kilimanjaro.

"Unapoenda katika eneo la tukio unapata fursa ya kuona hali halisi ya mambo yalivyo, kuliko kukaa ofisini na kusubiri taarifa kutoka kwa wasaidizi wako waliopo Wilayani, ambazo mara nyingi huwa na mapungufu mengi"

Aidha, katika ziara hiyo, Katibu Tawala amewaagiza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwa kushirikiana na Katibu Tawala wa Wilaya kuhakikisha wanaendelea na zoezi la kukusanya na kuandaa taarifa sahihi za idadi ya wananchi walioathirika na mafuriko hayo, lakini pia kukusanya taarifa zinazohusu mashamba yaliyoharibiwa na mvua kubwa zilizonyesha mkoani Kilimanjaro.

"Tunatambua kwamba wananchi wetu wanategemea shughuli za kilimo kama chanzo kikubwa cha chakula na mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao katika masoko. Ni vyema tukapata taarifa sahihi za mashamba yaliyoharibiwa na mvua ili serikali iweze kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kunusuru uchumi na maisha ya wananchi wa Wilaya ya Mwanga"

Hali kadhalika, Dkt Kazungu amewaagiza viongozi wa halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuendelea kumpa ushirikiano Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Mheshimiwa Thomas Apson katika jitihada za kuhamasisha wadau wa maendeleo Wilayani humo kutoa misaada ya hali na mali kwa wananchi waliokumbwa na athari za mvua kubwa zilizonyesha katika wilaya ya Mwanga.

Sanjari na hayo, Dkt. kazungu aliwafahamisha viongozi wa Wilaya ya Mwanga kuhusu jitihada zinazofanywa na Sekretariati ya Mkoa, chini ya Uongozi wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Dkt. Anna Mghwira katika kuhamasisha wadau wa maendeleo kutoa misaada ya hali na mali kwa wahanga wa mvua kubwa zilizonyesha mkoani hapa. Baadhi ya wadau wa maendeleo ambao wamekwishatoa misaada ni pamoja na Shirika la Red Cross pamoja na Kampuni ya uzalishaji vinywaji baridi ya Bonite.

Aidha, katika ziara hiyo, Dkt.Kazungu ametoa maelekezo kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuhakikisha wanasimamia utengenezaji wa miundombinu ya maji ya mvua katika katika kijiji cha Kileo. Katika kufanikisha hilo, Dkt. Kazungu amewataka viongozi wa Kijiji cha Kileo kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa kutosha ili kutatua tatizo la mafuriko, ambayo chanzo chake, kwa kiasi kubwa yanasababishwa na usimamizi hafifu wa miundo mbinu ya maji ya mvua.

Kadhalika, Dkt. Kazungu ametoa maelekezo kwa viongozi wa halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuhakikisha wanafanya kazi kwa ukaribu na Wakala wa Barabara za Mijini na vijini (TARURA) ili kurekekebisha kasoro zilizopelekea kuharibika kwa miundo mbinu ya barabara katika wilaya hiyo.

Serikali Mkoani Kilimanjaro kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeshatoa misaada ya vyakula kama vile unga wa sembe, maharage, sukari na mafuta ya kupikia kwa wahanga wa mafuriko. Misaada mingine ni pamoja na mablanketi, mashuka pamoja na vyandarua.

Shaban A. Pazi
Afisa Habari
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Kilimanjaro
27/04/2020